Maisha ya raha

hadi uzeeni



Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Maisha marefu, marefu sana!

Sisi ni wageni tu duniani.
Kuwa na umri mkubwa au kuzeeka?

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Maneno ya faraja
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Hauko peke yako
- Mafundisho ya Yesu Mlimani
- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Yesu na wanyama
- Hili ni Neno Langu A na Ω
- Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu ni neema ya Uzima



First Edition in Swahili: August 2023
1ère édition en Swahili: Août 2023

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents

Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Ni ukweli kwamba umri wa mwanadamu unasonga mbele siku baada ya siku.Hata hivyo, kuzeeka ni matokeo ya mawazo na tabia mbovu.

Kukubali umri kunazuia mtu kuzeeka. Uzee unaanza wakati tunalalamika mara nyingi kuhusu shida ndogo na pia kubwa za maisha yetu ya kidunia.

Ujana sio tu kipindi katika awamu ya maisha ni tena mtazamo wa kiroho ambao hauhusiani na wakati au umri Fulani wa maisha. Umri wa mtu si kitu cha muhimu, cha muhimu ni jinsi anavyotumia maisha yake, hiyo ndiyo inayopewa uzito sana na inayomuonyesha kwa kiwango kipi yeye ni kijana kiroho au la.

Mwendo wa maisha yetu unatokana na fikra zetu. Kwa sababu tunageuka kuwa fikra zetu, hivi karibuni tunapokuwa na umri fulani.

Mtu anayezingatia tu maisha yake yeye mwenyewe ni mzee, hata awe na umri gani.

Mtu yeyote ambaye katika ujana wake na umri wa kati anatekeleza kwa dhati maadili ya juu na anajitahidi kuyaendeleza, atabaki mwenye nguvu na kijana hata katika umri mkubwa.

Ushauri kwa vijana: Msipotoshwe!

Mtu anayetaka kubaki mwenye bidii na mwenye moyo mkunjufu hadi umri mkubwa, lazima aendelee kujifunza na, licha ya yote, asipoteze lengo alilojipangia maishani mwake, kwa sababu wakati mtu anaposonga mbele kila mara, lengo hilo huchukua sura mpya sana.

Kuelewa hakika kwamba maisha ya duniani ni majifunzo ni mtazamo wa kiroho unaopangilia mwendo wa maisha yetu duniani, iwe katika ujana, iwe katika umri

wa makamo au uzeeni. Mtu aliyeacha kujifunza hawezi kukua kiroho.

Kwa mwanadamu na nafsi yake, maisha ni mageuzi endelevu. Kujifunza na kufikia fikra na mwenendo mpya na adilifu kunaacha nafsi iwe na nguvu na mwili uwe na ujana.

Kila mtu, awe kijana au mzee, angepaswa kukubali kwamba maisha ya dunia ni hatua ya kwanza tu kuelekea uzima safi sana na kwamba kifo ni njia tu inayoelekeza kwenye aina nyingine ya uwepo ambao nao pia ni uzima. Kunufaika na maisha, jambo ambalo vijana na wazee huzungumzia, siyo kuburudisha hisia za mtu kwa njia tofauti, bali ni kuwa na lengo la kufikia yaani kuishi maisha adilifu na kupiga hatua katika mwelekeo huo.

Kujifunza ni kufikia ujuzi wa mambo ulio wazi ndani mwako mwenyewe, kwa kutafuta kufikia lengo kuu la maisha ya mtu, na baadaye kutenda kwa kutekeleza ukweli

ambao mtu ameutambua tayari. Hayo yanatupa uhakika na uhuru wa kiroho na tena nguvu ya kusonga mbele kuelekea lengo hilo.

Kuishi kwa dhamiri kunamaanisha kujifunza kwa dhamiri, kuwa na mtazamo mzuri kuhusu kila kipindi cha maisha ili kufaidika kiroho nacho. Kwani hali ya maisha ya juu kimaadili tunayoweza kuendeleza kwa msaada wa umri wetu, haitegemei tu umri wetu, bali pia mtazamo wetu wa kiroho. Mtu aliyeacha kujirekebisha mwenyewe hawezi kukuza kamwe maadili wala kuweza kukomaza matunda mazuri na kuyaleta ndani ya jamii.

Ni maisha adilifu tuliyoishi tu ndiyo iliyo muhimu, bali si anasa ya maisha ya duniani.

Umri mkubwa pia unatupa fursa nyingi, hasa wakati shinikizo la mafanikio ya kitaaluma inakwisha.

Wakati tamaa na mapenzi yao vinatulia na umri wao unawaomba wawe na utulivu mwingi wa kiriho, watu wengi wanaweza hivyo kugundua taaluma na ujuzi uliokuwa umejificha ndani mwao hadi hapo na kukuza taaluma hizo, pia wakitaka, wanaweza kuzitumia kwa manufaa ya majirani wao.

Uzima ni Mungu. Maisha adilifu tuliyoishi hutulinda na udhaifu na upweke katika uzee.

Tuachane na mambo ya zamani! Tushike njia kuelekea nchi takatifu! Kwa maneno mengine: Tubadilishe maisha yetu!

Tukifanikiwa kuchukua mabadiliko hayo ya maisha yetu kama fursa ya kuona mambo kupitia mtazamo mwingine, basi hakika tutapata mawazo na uwezekano wa kutoa mwelekeo mpya na bora kwa maisha yetu. Maazimio mazuri inayotushika moyoni tangu siku nyingi lakini ambayo maisha yetu ya

awali haikuturuhusu kufikia, sasa yanapata bahati ya kufikiwa. Hebu tuonyeshe nia thabiti, na haraka, matumaini mapya yatajitokeza, yakiambatana na imani kwamba mambo yatakuwa bora.

Sisi wenyewe tuna maisha na takdiri yetu mikononi mwetu. Hebu tuchukue fursa hiyo mpya! Hilo ni jambo la maana na siyo tu hapa na sasa, siyo tu kwa ajili ya maisha haya ya kidunia. Mambo mengi yanaweza tena kubadilika, kabla ya yote sisi wenyewe tunaweza kubadilika! Mtaona jinsi kuwapa wengine furaha bila ubinafsi kunamleta mtu furaha na raha.

Kwa upekee unapokuwa na umri fulani, kuwapa umuhimu wengine na kumhudumia jirani bila ubinafsi ni sifa nzuri inayoweza kukuzwa na kuboreshwa. Ikiwa mtu wa umri mkubwa anafahamu hayo na kuifanya tabia yake ya msingi, basi ana ufunguo wa

maisha tajiri mikononi mwake, pia hadi ukongwe. Basi maisha «humlipa» kwa namna yake: anapata mengi, maisha marefu, kama jinsi hayo ilivyosemwa tayari. Kwa sababu kuendelea kujifanya mwenye manufaa katika umri mkubwa kunatajirisha mtu kiroho.

Tuwe tayari kwa mabadiliko kiroho! Hayo yanawezekana ikiwa hatutaacha kujifunza kwa dhamiri, kwani kila siku, hakika, hutupa majukumu tofauti. Yeyote ambaye – kupitia uaminifu wake wa ndani kwa Uzima – anayakubali, pia atafanikiwa kumudu majukumu hayo. Kwa kuwa Mungu katika mambo yote ni msaada, ushauri, jibu, suluhu na anajua sana jinsi ya kuwaongoza wanae wanadamu.

Tukitambua mapema sana kwamba sisi ni wageni tu Duniani, basi hatutaridhika na tabia za zamani za uvivu zinazotawala watu wengi. Mtu mwenye dhamiri ya jambo hilo

atageukia daima ndani mwake,upande wa kiini cha kati cha nafsi, ambamo Mungu anakaa, kwa sababu anafahamu kwamba Mungu ni upendo, urembo, usafi, haki, na ni uzima wa milele.

Kutokana na ujuzi huo, na hekima hiyo, mtu anayeheshimu kila siku Kanuni kuu, «Jambo usilotaka kutendewa, usilitendee mtu mwingine», atatajirisha maisha yake. Mungu yupo hapo daima kwa ajili yetu, kwa kila mmoja kwa upekee, kwa sababu sisi ni wanae.

Mtu anayefuata maishani mwake kanuni za maadili ya Yesu, ya Kristo, anaweza kusema: Uzima ni wa milele. Katika Kristo mimi ni uzima wa milele.

Kwa kweli, hakuna mtu aliye mpweke. Mungu, Roho wa Baba yetu wa Milele, yumo ndani mwetu.

Mtu anayeyajua hayo ni shujaa, hakubali kutawaliwa na udhaifu wa kibinadamu.

Kutokana na dhamiri ya nguvu, ya upendo na hekima ya milele, anajilazimu kutenda tu yaliyo mema. Hivyo ana uwezo wa kumtumikia Mungu na kuwatumikia jirani zake, na kutimiza kazi za upendo usio na ubinafsi. Nguvu, upendo na hekima ya Mungu vitamsaidia katika hali yoyote. Mtu anayeshika Amri Kuu pia ana ufunguo wa maisha halisi.

Unaweza kuondoa «uchafu» wote uliorundikwa kwenye njia yetu ya uzima kama vile pia vikwazo, kwa kutubu, kurekebisha maovu na kutorudilia tena maovu yale yale, ili Roho wa milele, ambaye ni upendo, apate kutusaidia na kutuongoza.

Hebu tumwombe basi Kristo msaada! Yeye, aliye na upendo na anayependa sana kusaidia kila mmoja wetu, ataongezea nguvu hisia zetu chanya, zinazolingana na mapenzi ya Mungu, na atachochea hisia nzuri za uzima wetu wa kiroho, wa kiwango cha juu. Hata hivyo, ni wajibu wetu kuchukua uamuzi

wa kupiga hatua na kurekebisha kile kinachohitajika kurekebishwa. Kristo haingilii kamwe kati uamuzi huru wetu, ambao ni sehemu asilia ya urithi wetu wa milele.

Hebu tuelewe kwamba hofu ya magonjwa inayoweza kutupata hakika husababisha ugonjwa. Kwa hiyo tunapaswa kujizoeza kujaza moyo wetu na imani kwa Mungu, wa Milele, na kujiweka huru toka fikra za woga, wivu na chuki.

Uwe jasiri! Geukia kila siku, kila mara ikiwezekana, upande wa Roho asiye na mwisho, Roho wa upendo na wa huruma ndani mwako. Anajua mahitaji yako. Anajua madhaifu na sifa zako. Omba na jikabidhi Kwake! Mwangwi kutoka ndani ya nafsi yako ni uhuru, furaha, usafi na heshima. Hilo ni jibu la Mungu. Hofu ya wakati ujao, kwa mfano hofu ya upweke, hofu ya shida na matatizo, basi itabadilika kuwa hisia ya

usalama, ambayo pia nayo, inatokea ndani mwako kabisa wewe mwenyewe, kutoka kwa wa Milele aliye na maisha yako mikononi mwake – Yeye Baba wa umilele.

Laiti tungezungumza na mioyo ya vijana na kusema: Tumia kwa manufaa yako kila kipindi cha maisha yako ili ufikie ukuaji na upevu wako wa kiroho! Kwa sababu ukomavu wa kiroho huleta furaha na ukamilifu katika uzee.

Kila mtu amepewa kila mchana ili apate kufahamu mambo ya maisha yake – ambayo mchana huo unamuonyesha – na aichunguze ili apate yaliyo mema ndani mwake, ili ayaimarishe na kuyaendeleza. Kwa mtu anayetaka kuishi hivyo, matokeo ni kwamba kila mchana unajaa nguvu. Mchana haujui uchovu, tofauti na hayo unaletea nguvu mpya hatua inayofuata kuelekea uzima halisi, hatua hiyo tunapaswa kuipiga leo.

Udhaifu na ukosefu wa nguvu ya mwili mara nyingi ni alama ya tendo la kukubali mambo jinsi yalivyo, tendo la kukataa kuchukua shida za maisha kama jambo la kufanyia kazi na la kutolea suluhisho – kukubali badala ya kufikiria kwa kiburi kuwa matukio na wengine ndio wanapaswa kubadilika.

Tendo la kuzeeka kulingana na maisha ya kiroho si balaa! Yeyote anayefanya azimio la kujihisi kwamba anazaliwa upya kila mchana kwa kukubali mchana wake jinsi ulivyo, huyo atahisi mkondo wa nguvu ya uzima ulio katika mchana huo.

Moyo wa mtu anayeishi maisha kwa uangalifu unaanza kupiga kwa kina sana. Dhamiri ya umoja inajitokeza ndani mwake kupitia hisia ya furaha yenye kujaa upendo wa ndani. Mtu huyo anafanya kila awezalo kuwasaidia wanyama walio katika dhiki na pia majirani zake wanaoishi katika wasiwasi

na matatizo. Anaona mazingira katika uzuri wake wote, anaifurahia na kuhisi humo pumzi ya Roho muumba, pumzi ambayo pia inavuma ndani sana ya mtu anayeelekea upande wa umoja. Hayo yanafanya mtu awe na heshima ya uzima, ambao ni Mungu, na furaha ya kuishi, kwa lengo la kuhudumia viumbe.

Hamu ya kuomba kwa wazee wengi hujitokeza. Hapa pia, ni suala la kujifunza, suala la kujifunza kuomba na siyo kutamka sala zilizoandaliwa tayari. Kuomba kunamaanisha kubadilika, yaani kutenda ili sala igeuke kuwa maisha. Mtu anayeomba hivyo hahitaji kanisa lililojengwa kwa mawe, bali anahitaji chumba kidogo chenye ukimya, kama alivyoagiza Yesu, Kristo, kusudi aingie kwa kimya nafsini mwake, ndani ya patakatifu pa patakatifu nafsini panapong'aa.

Kuomba kwa imani ya kina kunamaanisha kuwa kimya, kwa sababu sala yenye kujaa Imani huzaa matumaini na kujitoa kwa

Mungu. Kutegemea kabisa chemchem kuu isiyokauka ya nuru ndani mwetu, kutegemea kile kilicho kitakatifu sana nafsini mwetu, kunamsaidia mtu anayeomba kwa kweli, kwani maisha yake yanageuka utimilifu wa sala zake. Maisha iliyo na mwelekeo wenye dhamiri husababisha maisha ya raha. Basi, siku mbovu na za giza za zamani hupotea. Kwa yule anayesali, nuru inang'aa sana, inaonekana zaidi, kiasi kwamba ndani mwake anazingatia lengo hili: ninaendelea kuelekea kwenye uzima wa kiwango cha juu, kuelekea upanda wa Uzima safi.

Vijana wengi wanatarajia hekima kutoka kwa watu wenye umri mkubwa, hekima inayotokana na umri, hekima isiyo na shinikizo na isiyotafuta kuwa sahihi kwa gharama yoyote. Hekima ya kweli ni utajiri wa uzoefu ambao mtu alipata na unaotuwezesha kuelewa kwa kina ukweli wa maisha, matukio na utu wa mwanadamu. Mtu mwenye hekima ya kweli humwacha jirani huru. Anawasiliana naye kupitia sheria ya uamuzi huru isiyote-

gemea mtu, anawasiliana naye kwa uvumilivu, upole na ukarimu. Mtu mwenye hekima anajua kunyamaa kwa wakati muafaka na kwa wema. Mtu mwenye hekima hapendelei watu kulingana na thamani yao na haukumu kamwe.

Msomaji wa kitabu kidogo hiki aliye makini atatambua kwamba si umri ndicho kitu cha muhimu bali ni mtazamo wa mtu kuhusu uzima.

Uwe na mtazamo mzuri na utahisi mengi, utahisi uzima tele!

Kuzeeka ni mojawapo ya kanuni za dunia. Hata hivyo, mtu anayefahamu wajibu wa maisha yake hatazeeka katika umri mkubwa. Kila mtu huja ulimwenguni na jukumu kwa maisha haya. Hatua tofauti za kazi hiyo hujifunua kwake siku baada ya siku. Heri yule anayezijali, maana hivyo anakomaa!

*M*tu anayetegemea umoja na heshima ya Kanuni yenye thamani maishani mwake hatamchukia kamwe jirani yake; wala hatawaua wanyama, wala kula nyama zao, wala hatatenda jeuri yoyote dhidi ya Ardhi-Mama. Watu walio na dhamiri hiyo hawatakuwa kamwe watu wabinafsi na wataonja hadi uzee utamu wa maisha ya kiroho na siku zao watazijaza na raha hiyo – na kujaa uzima tele.






Roho huru – Mungu ndani mwetu

Kitabu hiki kinamwelekeza msomaji kwenye njia ya uhuru na kinamuwezesha kujitenga na imani potovu, mila ngumu na taasisi zinazotushikilia. Njia hiyo ni njia iongozayo kwa Mungu, kwa Mungu ndani mwetu.

S179SW • ISBN 978-3-96446-247-3 • Kurasa 76



Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake.

S170SW • ISBN 978-3-96446-226-8 • Kurasa 46



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi inahitaji mafunzo. Kwa kuwa sala halisi tunayoifanya ndani mwetu wenyewe ni mazungumzo na Mungu.

S174SW • ISBN 978-3-96446-225-1 • Kurasa 54




Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote.

S338SW • ISBN 978-3-96446-227-5 • Kurasa 46

Vitabu vingine vinapatikana katika lugha ya Kiswahili, kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi tena

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
www.gabriele-publishing.com



Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com